BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 02 Oktoba, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2022/2023.

### Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2022/2023.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Bajeti Kuhusu Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango juu ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Ripoti ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

6. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

   Je, sababu zipi zinazopelekea kesi nyingi za madawa ya kulevya kuchelewa kusikilizwa na kupatiwa hukumu katika Mahakama zetu licha ya kuwa watuhumiwa wa kesi hizo hukamatwa wakiwa na vidhibiti halisi vya madawa hayo.

74. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

    Kuna baadhi ya taasisi zinakosa ufanisi kutokana na uhaba wa wafanyakazi kwa baadhi ya kada.

    Je, Serikali ina mkakati gani wa kuipatia ufumbuzi changamoto hiyo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

107. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

     Je, ni lini Serikali itaanzisha Benki ya Uwekezaji nchini ili iweze kuwasaidia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

**Wizara ya Afya:**

77. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kwa kuwa hospitali ya Chukwani inatoa huduma za afya kwa muda wa masaa ishirini na nne. Na kwa kuwa Serikali kupitia Wizara ya Afya ilifanya ukarabati mkubwa sana wa hospitali hiyo, kwa lengo la kuboresha huduma za afya kwa wananchi hasa walio karibu na hospitali hiyo. Na kwa kuwa ukarabati huo bado haujakamilika huku huduma za afya zikiendelea kutolewa, lakini kukiwa na uhaba wa baadhi ya vitendea kazi na dawa.

    Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kuimaliza changamoto hiyo katika hospitali ya Chukwani.

78. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

    Kituo cha Afya cha Chukwani kinahudumia shehia zaidi ya mbili lakini kipo katika hali hatarishi na kina uhaba mkubwa wa vitendea kazi. Katika kuwapa matumaini wananchi, Wizara ya Afya iliahidi kukikarabati kituo hicho, ingawa ahadi hiyo haijatekelezwa hadi leo hii.

    Je, ni lini Serikali itaitekeleza ahadi hiyo.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

100. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

     Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kufanikisha mashindano ya Kombe la Mapunduzi la kuadhimisha miaka 59 ya Mapinduzi. Katika kujiandaa na mashindano yajayo ya miaka 60, maandalizi yamekuwa mazuri mpaka hivi sasa.

     Je, katika maandalizi hayo kuna mpango wa kuyatanua zaidi mashindano ya Kombe la Mapunduzi kwa kuvialika vilabu vikubwa vya soka kutoka nchi jirani za Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

97. MHESHIMIWA MWANAASHA KHAMIS JUMA (Jimbo la Dimani)- Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Matukio ya ajali za barabarani kwa wanafunzi wa ngazi ya Maandalizi na Msingi yamekuwa yakiongezeka sana katika siku za hivi karibuni. Vifo na majeruhi wameripotiwa sana kwenye vyombo vya habari, hali inayoleta wasiwasi kwa wazazi na walezi.

(a) Je, Wizara yako imechukuwa hatua gani ya kudhibiti hali hiyo ili kuwanusuru watoto wetu na matukio ya ajali za barabarani.

(b) Kwa kushirikiana na Mamlaka nyengine, je, Wizara haioni haja ya kuweka Mpango wa Usalama Shirikishi wa Barabarani kwa kila shehia kwa kuwepo watu wa kujitolea wa kuwasaidia watoto kuvuka barabara pale wanapokwenda na kurudi skuli.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo Ndogo kwa mwaka 2022/2023.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

Ripoti ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango Kuhusu Ripoti ya Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwa mwaka 2022/2023.

**Zanzibar,**
**02 Oktoba, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA.**